



INDEPENDENT ELECTORAL AND BOUNDARIES COMMISSION (IEBC)

**UJUMBE KWA
MPIGA KURA
KWENYE UCHAGUZI
MKUU 2022**

1.0 UCHAGUZI WA 2022

Uchaguzi mkuu utafanyika tarehe 9/8/2022 katika maeneo yote 290 nchini.

2.0 IDADI YA WAPIGAKURA NCHINI

Idadi ya wapigakura nchini ni **Milioni ishirini na mbili, Elfu mia moja na ishirini, mia nne na hamsini na wanane (22,120,458).**

3.0 STAKABADHI ZA KUPIGIA KURA


Ni lazima mpiga kura awe na stakabadhi aliyoitumia kujiandikisha kuwa mpigakura ili kushiriki katika uchaguzi huu. Stakabadhi hizo ni:

- (i) Kitambulisho halisi cha Kenya au
- (ii) Pasipoti ya Kenya.

4.0 SAA ZA KUFUNGUA NA KUFUNGA VITUO VYA KUPIGIA KURA

Vituo vyote vya kupigia kura vitafunguliwa saa kumi na mbili asubuhi na kufungwa saa kumi na moja jioni.

5.0 UTARATIBU WA KUPIGIA KURA



6.0 MWITO WA KUZUIA KUENEA KWA VIRUSI VYA COVID-19

Kwa mujibu wa maagizo ya Wizara ya Afya kuhusu COVID-19, Mpiga kura LAZIMA:

- (i) Avae barakoa inayofunika pua na mdomo kabla ya kuruhusiwa katika kituo cha kupigia kura.
- (ii) Apimwe kiwango cha joto ya mwili wake katika lango la kituo cha kupigia kura.
- (iii) Anawe mikono yake kwa sabuni au atumie kieuzi katika lango la kituo cha kupigia kura.
- (iv) Adumishe umbali wa mita 1.5 akiwa kwenye foleni ya kupigia kura.

7.0 NJIA ZA KUWATAMBUA WAPIGIA KURA

Kila mpiga kura atatambuliwa kupitia mtambo wa KIEMS kwa kutumia:

- (i) Alama za vidole.
- (ii) Iwapo kutakuwa na changamoto kumtambulisha mpiga kura kwa kutumia alama za vidole, Nambari ya Kitambulisho au Pasipoti itatumika kumtambua mpigakura husika ndani ya Mtambo wa KIEMS.

8.0 USAIDIZI KWA MPIGAKURA

Mpigakura anaweza kusaidiwa kwa njia zifuatazo:

1. Mpigakura kuja na msaidizi wake ambaye:
 - (i) Ni Mkenya wa miaka 18 na zaidi.
 - (ii) Ana Kitambulisho au Pasipoti ya Kenya.
 - (iii) Atakula kiapo cha kuweka siri kuhusu chaguo la mpigakura aliyemsaidia.
 - (iv) Atamsaidia mpiga kura mmoja tu katika uchaguzi huu.
2. Mpigakura kusaidiwa na Afsa wa IEBC anayesimamia kituo cha kupiga kura huku mawakala/maajenti wa vyama/wagombeaji wakishuhudia.

9.0 KUWEKA ALAMA KWENYE KARATASI YA KURA KUMCHAGUA KIONGOZI UMTAKAYE

Baada ya mpigakura kutambuliwa, atapewa karatasi sita za kura:

- (i) Kisha ataenda kwenye kizimba cha kupigia kura ili kumchagua mgombeaji anayetaka kwa kutumia alama tu kwa kila karatasi.
- (ii) Mpigakura atawekwa wino kwenye kidole chake baada ya kupiga kura.
- (iii) Mpigakura atahitajika kuondoka kituoni baada ya kukamilisha shughuli ya kupiga kura.



SAMPULI ZA ALAMA SAHIHI KWENYE KARATASI ZA KURA

1 **PRESIDENTIAL BALLOT (WHITE)**
INDEPENDENT ELECTORAL AND BOUNDARIES COMMISSION
BALLOT PAPER: PRESIDENTIAL ELECTION

WHICH CANDIDATE DO YOU WANT TO ELECT?

Presidential Candidate	Candidate's Photo and Name	Mark Your Ballot Here
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input checked="" type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>

2 **MEMBER OF NATIONAL ASSEMBLY BALLOT (GREEN)**
INDEPENDENT ELECTORAL AND BOUNDARIES COMMISSION
BALLOT PAPER: MEMBER OF NATIONAL ASSEMBLY

WHICH CANDIDATE DO YOU WANT TO ELECT?

Member of National Assembly Candidate	Candidate's Photo and Name	Mark Your Ballot Here
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input checked="" type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>

3 **COUNTY ASSEMBLY WARD BALLOT (BEIGE)**
INDEPENDENT ELECTORAL AND BOUNDARIES COMMISSION
BALLOT PAPER: COUNTY ASSEMBLY WARD ELECTION

WHICH CANDIDATE DO YOU WANT TO ELECT?

County Assembly Ward Candidate	Candidate's Photo and Name	Mark Your Ballot Here
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input checked="" type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>

4 **SENATOR'S BALLOT (YELLOW)**
INDEPENDENT ELECTORAL AND BOUNDARIES COMMISSION
BALLOT PAPER: SENATE ELECTION

WHICH CANDIDATE DO YOU WANT TO ELECT?

Senator Candidate	Candidate's Photo and Name	Mark Your Ballot Here
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input checked="" type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>

5 **COUNTY WOMAN MEMBER OF NATIONAL ASSEMBLY BALLOT (PURPLE)**
INDEPENDENT ELECTORAL AND BOUNDARIES COMMISSION
BALLOT PAPER: COUNTY WOMAN MEMBER OF NATIONAL ASSEMBLY ELECTION

WHICH CANDIDATE DO YOU WANT TO ELECT?

County Woman Member of National Assembly Candidate	Candidate's Photo and Name	Mark Your Ballot Here
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input checked="" type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>

6 **GOVERNOR'S BALLOT (BLUE)**
INDEPENDENT ELECTORAL AND BOUNDARIES COMMISSION
BALLOT PAPER: GOVERNOR ELECTION

WHICH CANDIDATE DO YOU WANT TO ELECT?

Governor Candidate	Candidate's Photo and Name	Mark Your Ballot Here
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input checked="" type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>
	WILSON KIPKORIR	<input type="checkbox"/>

10.0 HISANI KWA WAPIGAKURA WENYE MAHITAJI SPESHILI

Wapigakura wenye mahitaji speshili ni kama wamama wajawazito na walio na watoto wadogo, wagonjwa, walemavu na wakongwe. Tume inahimiza wapigakura wote kuruhusu maafisa wa IEBC kuwafanyia hisani hawa wapigakura ili kuwawezesha kupiga kura kwa haraka.

11.0 KUTUMBUKIZA KARATASI ZA KURA KWENYE SANDUKU

- (i) Mpigakura anahitajika kutumbukiza kila karatasi ya kura kwenye sanduku yake.
- (ii) Kila kifuniko cha Sanduku ina rangi sawa na karatasi ya kura kama inavyoonyeshwa kwenye mbango hii.

12.0 KUTANGAZA MATOKEO YA CHAGUZI MBALIMBALI

Matokeo ya kura yatatangazwa kwa viwango vinne:

- (i) Kwenye kituo cha kupiga kura.
- (ii) Kwenye ukumbi wa kujumlisha kura katika maeneo bunge 290.
- (iii) Kwenye ukumbi wa kujumlisha kura katika Kaunti zote 47.
- (iv) Kwenye ukumbi wa kitaifa wa kujumlisha kura za Rais.

13.0 WATU WANAORUHUSIWA KWENYE VITUO VYA KUPIGIA KURA NA KUMBI ZA KUJUMLISHA KURA

Watu wafuatao wana ruhusa ya kuingia katika vituo vya kupigia kura na kwenye kumbi za kujumlisha kura:

- (i) Maafisa wa IEBC.
- (ii) Maafisa wa Usalama.
- (iii) Mawakala/Maajenti wa Vyama/Wagombeaji.
- (iv) Afisa Msimamizi wa Kituo/Makarani wa uchaguzi.
- (v) Afisa Mdogo wa kituo.
- (vi) Waangalizi walioidhinishwa.
- (vii) Mtu yeyote aliyeidhinishwa na IEBC.

14.0 MWITO WA TUME YA IEBC KWA WAPIGAKURA

Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) inawahimiza wapiga kura wote katika maeneo ya uchaguzi kuwa:

- (i) Wajitokeze kwa wingi kumchagua kiongozi wao.
- (ii) Wafike mapema katika vituo vya kupiga kura.
- (iii) Wadumishe amani kabla ya, wakati wa, na baada ya kupiga kura.
- (iv) Waondoke katika vituo vya kupiga kura baada ya kupiga kura.
- (v) Wasitishie kampeni zote masaa 48 kabla ya kura kupigwa.
- (vi) Waripoti ukiukaji wa aina yeyote wa sheria kwa maafisa wa polisi, Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa kituo cha uchaguzi.
- (vii) Wawasilishe mahakamani malalamishi yanayotokana na matokeo ya uchaguzi (ikiwa yapo).

INDEPENDENT ELECTORAL AND BOUNDARIES COMMISSION (IEBC)

University Way, Anniversary Towers, 6th Floor,
P.O. Box 45371 - 00100 Nairobi, Kenya. • Tel: (254) 020 - 2769000/2877000
Email: info@iebc.or.ke • Website: www.iebc.or.ke



@IEBCkenya



IEBCKenya



IEBCKenya



IEBCKenya

Your Vote, Your future.